

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

612

URAIA

Muda: Saa 3

Mwaka : 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

110612 100024

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia hoja nne, ainisha majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Fikiria umepangiwa kufundisha mada ndogo ya *Haki za Raia* kwa wanafunzi wa Darasa la Sita. Ni mambo gani utakayoyasisitiza juu ya umuhimu wa kuzingatia haki za raia katika Dola? Toa hoja nne.
3. Kwa kutumia hoja nne, bainisha mila zinazochangia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI katika jamii za Kitanzania.
4. Eleza kwa kifupi umuhimu wa utaalamu katika ukuaji wa uchumi nchini Tanzania. Toa hoja nne.
5. Kama mwalimu mahiri wa somo la Uraia, elezea kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mada inayofundishwa.
6. Nini umuhimu wa Muhtasari wa somo la Uraia kwa mwalimu tarajali anayejiandaa na mafunzo kwa vitendo? Toa hoja nne.
7. Fikiria umepangiwa kufundisha somo la Uraia katika shule ya msingi baada tu ya kuhitimu mafunzo yako ya Ualimu. Ni mbinu zipi utakazotumia katika kupata zana za kufundishia na kujifunzia? Toa hoja nne.
8. Kwa kutoa mifano, elezea dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika azimio la kazi la somo la Uraia:
 - (a) Vitendo vya ufundishaji.
 - (b) Vitendo vya Ujifunzaji.
9. Kuna umuhimu gani kwa mwalimu tarajali kuchunga mwenendo wake anapokuwa katika mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu? Toa hoja nne.
10. Ni kwa namna gani tathmini endelevi hutofautina na tathmini tatuji?

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Chambua vikwazo vitano dhidi ya utawala wa kidemokrasia katika nchi.

12. Fikiria umeteuliwa kumuwakilisha Mkuu wako wa shule kwenye kikao cha maadili katika Wilaya yenu. Ni hoja zipi utakazozitoa kama njia zinazoweza kutumika katika kudumisha maadili mema kwa jamii? Toa hoja tano.
13. Kwa kutumia hoja sita, eleza ni kwa namna gani Msingi wa Kutofungamana na Upande Wowote unainufaisha Tanzania katika utekelezaji wa sera yake ya Mambo ya Nje.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. “Stadi ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa ni muhimu kwa mtu kuwa raia mwema.” Tetea kauli hii kwa kutoa hoja tano.
15. Kwa kutumia maarifa uliyopata katika mafunzo yako ya Ualimu, fafanua madhumuni sita ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundishia somo la Uraia.
16. Kwa kutumia hoja tano, eleza namna zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia zinavyoweza kutunzwa.